**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA KWANZA

**06 NOVEMBA, 2018**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 06 NOVEMBA, 2018

**I. WIMBO WA TAIFA:**

**II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA TATU ASUBUHI:**

**III. KIAPO CHA UAMINIFU:**

Orodha ya Wabunge wanaoapishwa.

1. Mhe. Julius Kalanga Laizer;
2. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara;
3. Mhe. Timotheo Paul Mnzava; na
4. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka.

**IV. TAARIFA YA SPIKA:**

## V. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## VI. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**1. MHESHIMIWA ESTHER MICHAEL MMASI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Ukosefu wa ajira bado ni changamoto kubwa hasa tunapoangalia takwimu za kidunia na hata katika nchi yetu:-

(a) Je, Serikali imejipangaje katika kulinda ajira za Vijana kupitia Sera ya Ajira;

(b) Kwenye kada ya TEHAMA nchi yetu imekuwa ikipoteza nafasi nyingi za ajira kwa Vijana kwenye taasisi za kifedha kwa kazi nyingi kupelekwa nje ya nchi ikiwemo nchi jirani. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto hii.

**2. MHESHIMIWA ABDALLAH ALLY MTOLEA (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Tarehe 9 Desemba, 1961 Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere alisema tutauwasha Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro ili umulike nchi nzima na kuleta upendo, amani n.k.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Je, utaratibu huu wa kukimbiza Mwenge nchi nzima kila mwaka umetoka wapi.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**3. MHESHIMIWA ENG. CHRISTOPHER KAJORO CHIZA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Sera ya Serikali ni kuwa na Hospitali ya Wilaya na Vituo vya Afya katika kila Kata:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kakonko;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya katika Kata za Kiziguzigu, Kasanda, Gwarama, Rugenge, Nyamutukiza na Kata nyingine ambazo hazina Vituo vya Afya.

**4. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIAH BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la Wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Bukoli.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

5. **MHESHIMIWA EDWARD FRANZ MWALONGO (NJOMBE MJINI):**

   Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Hospitali ya Kibena ni kongwe na imechakaa sana:-

   Je, ni lini Serikali itaifanyia ukarabati.

**WIZARA YA KILIMO:**

6. **MHESHIMIWA BALOZI ADADI MOHAMED RAJAB (MUHEZA):**

   Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Chuo cha Kilimo cha Utafiti cha Mlingano Wilayani Muheza kipo katika hali mbaya:-

   Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye Chuo hicho ili kiweze kufanyiwa ukarabati.

7. **MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

   Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Wakulima wengi wamehamasika katika Kilimo

cha Alizeti lakini Alizeti inayolimwa haitoi mafuta kwa wingi:-

Je, Serikali ina mkakati gani katika kuimarisha utafiti wa mbegu ya alizeti inayotoa mafuta mengi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**8. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mji Mkongwe wa Mikindani uliopo katika Manispaa ya Mtwara Mikindani unakuwa kivutio cha utalii.

**9. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Mwaka 2017 wakati Mhe. Rais akiwa katika ziara Mkoa wa Kigoma, katika Wilaya ya Kasulu aliwaruhusu Wananchi waliokuwa wakilima katika maeneo ya Hifadhi ya Makere (Kagera Nkanda) kwa sharti kwamba wasiongeze maeneo mengine zaidi ya yale waliyokuwa wakilima:-

Je, kwa nini TFS wanapingana na agizo la Mhe. Rais na wanawatesa Wananchi kwa kuwapiga na kuwanyang'anya baiskeli na pikipiki.

**WIZARA YA NISHATI:**

**10. MHESHIMIWA AUGUSTINO VUMA HOLLE (KASULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Kwa muda mrefu Mkoa wa Kigoma umesubiri kuunganishwa kwenye Grid ya Taifa ya umeme:-

Je, ni lini Serikali itaunganisha Mkoa huo kwenye Grid ya Taifa ya umeme.

**11. MHESHIMIWA MUSA RASHID NTIMIZI (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Katika mradi wa kupeleka umeme Vijijini, Jimbo la Igalula limepitiwa na umeme katika baadhi ya maeneo ya Kata za Kigwa, Igalula, Goweko na Nsolola tu kati ya Kata kumi na moja za Jimbo hilo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Kata na Vijiji vya Jimbo la Igalula vilivyobaki;



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA
UHURU NA UMOJA

(b) Katika Kata ya Igalula, Kijiji cha Igalula ambapo kuna bwawa la maji kuna hitaji la nguzo kumi tu kwa ajili ya kusaidia kusukuma mitambo ya maji; Je, Serikali itasaidiaje kupeleka nguzo hizo ili kutatua tatizo hilo.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**12. MHESHIMIWA PETER AMBROSE LIJUALIKALI (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

(a) Je, ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara umefikia hatua gani;

(b) Je, barabara hiyo inatarajiwa kukamilika lini.

**13. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN KAUNJE (LINDI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- TANROADS ilifanya upanuzi wa *"Road Reserve"* tangu mwaka 2011 ambayo ilihusisha tathmini ya mali zilizopo kwenye maeneo husika:-

Je, ni lini Wananchi wa Lindi watalipwa fidia zao.

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

**14. MHESHIMIWA MARIA NDILLA KANGOYE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Serikali katika Ilani ya Uchaguzi iliahidi kuboresha huduma ya maji kwa Vijiji kutoka asilimia 67.7 kwa mwaka 2015 hadi asilimia 85 kwa mwaka 2020 na kwa upande wa Mijini asilimia 68 kwa mwaka 2015 hadi asilimia 95 kwa mwaka 2020:-

(a) Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kutekeleza azma hiyo ambayo pia itasaidia kumtua ndoo kichwani Mwanamke;

(b) Je, ni lini bwawa la Kidunda litajengwa ili kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam.

**15. MHESHIMIWA LATHIFAH HASSAN CHANDE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wananchi wa Mkoa wa Lindi wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kwa muda mrefu hadi kusababisha baadhi ya

Wananchi hasa wa Vijijini kutumia maji ya mito na mabwawa pamoja na mifugo:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi mbalimbali ya maji Mkoani Lindi;

(b) Je, ni lini Serikali itahakikisha upatikanaji wa maji safi katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi ili kuepusha uwezekano wa magonjwa ya mlipuko kwa wauguzi na wagonjwa.

## VII. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa Mwaka 2018 (*The Microfinance Bill, 2018*).

## VIII. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.

## IX. KAMATI YA MIPANGO:

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**06 NOVEMBA, 2018** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA